BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 01 Juni, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Afya:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2023/2024.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

153. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika kuhakikisha nchi inakuwa na amani, ni jukumu la Serikali kuvitumia vyombo vyake vya ulinzi lakini pia kuwashirikisha wananchi katika kushirikiana na vyombo hivyo, ili nchi izidi kuwa na amani.

Je, kuna mikakati gani ambayo Serikali inaichukua juu ya kuwashirikisha raia kutoa taarifa za kiusalama na uhalifu.

**<u>Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:</u>**

239. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Katika maeneo ya Kware ya Mkoani, kumekuwa na utitiri wa mashine za kusaga kokoto (crushers) zinazomilikiwa na Serikali. Kwa kuwa baadhi ya mashine hizi hutumia nishati ya diesel na hivyo kuzalisha hewa mkaa (carbon dioxide) ambayo ni hatari kwa afya za binaadamu sambamba na kuzalisha vumbi (dust).

(a) Je, huko si kuharibu mazingira.

(b) Je, Serikali itawasaidia vipi raia wake hao dhaifu ili kupambana na athari za kimazingira.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

124. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Matendo yanayoendelea Zanzibar kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) yanathibitisha kwamba sera na mfumo wa kitaasisi na wa kisheria wa udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na hasa uwekezaji na matumizi ya fedha za Mifuko hiyo haviko imara.

(a) Je, ni ipi tathimini ya Serikali na wadau kuhusiana na mwenendo wa ZSSF.

(b) Je, Serikali haioni ulazima wa kupitia na kurekebisha sera na mfumo wa kitaasisi na wa kisheria wa udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Zanzibar.

(c) Je, ni upi mlinganisho wa kimaslahi wa wanachama wa ZSSF na mifuko mengine ya Hifadhi ya Jamii Tanzania.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

152. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kutokana na kasi ya kukuwa kwa lugha ya Kiswahili duniani lugha yetu hii adhimu sasa imekuwa ni bidhaa ghali inayoweza kuinua pato la Taifa kupitia mapato mbali mbali yanayotokana na kukua na kuenea kwake. Miongoni mwa wenye majukumu hayo ni pamoja na Balozi zetu zinazotuwakilisha katika nchi mbali mbali duniani.

(a) Je, Serikali inazitumia vipi Balozi zetu kukikuza na kukieneza Kiswahili duniani.

(b) Je, ni nchi ngapi kupitia uwakilishi wa balozi zetu zimeanza mikakati ya kukibidhaisha Kiswahili.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

82. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Shehia ya Mwambe, Mchakwe, Jombwe na Shamiani hupata maji ya mfereji kutoka katika visima vilivyopo Kengeja, ingawa kwa muda mrefu sasa maji hayo hayapatikani vizuri na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa sasa imechimba kisima chengine ili kuongeza nguvu ya kupeleka maji katika shehia hizo. Hata hivyo, mpaka sasa kisima hicho hakijawekwa pampu na hali ya upatikanaji wa maji kwa sasa haiko vizuri.

(a) Je, Wizara yako ina ufahamu upi wa tatizo la maji katika shehia hizo.

(b) Je, lini tatizo hilo litapatiwa ufumbuzi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

134. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Mara kwa mara tumekuwa tunashuhudia uzinduzi wa meli mbali mbali za mwendo wa kasi zinazofanya safari Unguja na Dar - es - Salaam.

(a) Je, Serikali kupitia wawekezaji wetu hawa hawalioni tatizo la usafiri liliopo baina ya Unguja na Pemba.

(b) Je, Serikali inashindwa vipi kuwashawishi wawekezaji kulitatua tatizo hili.

(c) Je, Serikali haioni kuwa kwa sasa usafiri wa Unguja kwenda Dar – es – Salaam unatosheleza.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

151. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Miongoni mwa ubunifu unaofanywa na vijana wetu wa Zanzibar na unaoutangaza utalii wa nchi yetu, ni kitendo cha vijana wetu kupiga mbizi kwa staili inayovutia hapo Forodhani.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwatunza vijana wanaopiga mbizi hapo Forodhani ili kuzidi kuutunza utalii wetu duniani.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2023/2024.

**Waziri wa Afya:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**01 Juni, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**